


ISOME!!!
~~USISHIKE!~~
Shajara ya Paul
2017
TIME TO TALK!
#talkaboutchildwork

Mei 1

Mpendwa shajara!
Hatimaye tumehamia katika jiji,
mama, Trixi na mimi tu.
Sasa kila kitu kitakuwa bora.



Chumba changu
(ona ya nje mazingira
yanavyovutia!)



Mei 2

Mpendwa shajara, leo nilikwenda
kwenye ziara ya ugunduzi pamoja
na Trixi. Makazi ni makubwa sana
kwa matembezi. Nilichukua baiskeli ya
mama. Kiti chake kiko juu sana lakini,
ina kikapu kwa ajili ya Trixi.



Chora picha kwa ajili ya ya
mama kama zawadi ya siku
yake ya kuzaliwa ... labda kama
hii? Labda pamoja na fremu

Mei 3

Mpendwa shajara. Leo ilikuwa siku yangu ya
kwanza katika shule mpya na nilifanikiwa
kucheza mpira wa miguu wakati wa
mapumziko. Magoli matatu! Katika darasa
la Sanaa Bi Storm alisema picha yangu
ilikuwa nzuri sana na aliionyesha kwa kila
mtu. Niliona aibu! Ikiwa ninampenda
Amy Winehouse. Amy nani?

Labda Nimepata fremu kwa ajili ya picha ya Mama.
si mchezo au sio? Euros 49!! Hizo ni pesa za akiba kwa miezi
mitano! Ni kama, ni fedha bado. Si mchezo

Mei 4

Mpendwa shajara! Mwalimu wetu wa Siasa ni safi sana! Jina lake ni Maia. Sisi ni darasa lake la kwanza na yeye ni mwema sana. Leo tulijifunza kuhusu Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto. Ni aina ya kitabu cha sheria ambacho nchi zote zinahitajika kufuata. Vipengele vitatu ninavyovipenda kwenye mkataba huo ni: Mwambie Mama!

Kifungu cha 12: Watoto wote wana haki ya kuwa na maoni yao na watu wazima wanapaswa 'kutusikiliza *' na kuchukulia kwa uzito maoni yetu.

Kifungu cha 17: Simu, kompyuta, Televisheni vyote vinaruhusiwa kwa watoto, ili tuweze kujua mambo yatakayotusaidia kuwa na maisha mazuri.

*Hiyo inamaanisha simu kuipigia marufuku ni MARUFUKU, ndiyo!




Kifungu cha 37: Ni MARUFUKU kuadhibu watoto!

Ajira kwa watoto pia inatajwa Inatokea ulimwenguni pote, anasema Maia. Badala ya kwenda shule, watoto wengi wanafanya kazi kwa bidii na wanalipwa pesa kidogo au hawalipwi, na wanatendewa vibaya. Hivi karibuni kutakuwa na mkutano huko Argentina, ambapo wanakwenda kutoa ushauri jinsi ya kuwalinda watoto hawa vizuri, lakini watoto hawajakaribishwa Ni jambo la kushangaza sana, sio?

Mei 6

Mpendwa Shajara! Mvulana anaeneza vipeperushi kwenye ujirani. Nilijiuliza ninawezaje kupata kazi hiyo, pia. Anasema mimi ni mdogo sana, lakini mwishoni mwa wiki hii ninaweza kumsaidia. Atanilipa sehemu ya mshahara wake. Nitapata Euro 30! Ukiongeza na akiba yangu kiasi hiki kinatosha kununua fremu kwa ajili ya siku ya kuzaliwa kwa mama yangu!



Mei 7


Mpendwa shajara, kuanzia leo mimi ni mfanyakazi mtoto pia! Mara baada ya shule, mvulana alinipa toroli na mkakati. Niliweza kusambaza kwenye nyumba 13, na masanduku ya barua 312 karibu mitaa yote Mmoja wao aliuma mkono wangu.

Mei 8

Masaa 7, nyumba 295. Majarida 825 tu, na ilikuwa mvua! Nimechoka. Mama anadhani Nilikuwa nikicheza mpira wa miguu. Ninapaswa kukaa kitandani kesho, alisema.

Mei 9


Mpendwa shajara, nimeamka asubuhi na mapema na nikam-chukua Trixi ili asipige kelele na kumwamsha Mama. Saa 3 kwa vipeperushi 500 vya mwisho. 100 kati ya hivyo nilivitupa kuchakata, isingekuwa hivyo nisingemaliza. Nilirudisha toroli la yule mvulana, lakini alinipa euro 15 tu na akasema, "Euro nyingine 15 ni zangu kama asilimia faida... " Msaliti!



Supermaia alikuwa akiwawakilisha watoto wote wanaofanya kazi duniani, kama alivyoeleza. Alipenda kukutana na wengi wao iwezekanavyo na kujua wanafanya kazi gani, kwanini wanafanya kazi na kwa jinsi gani.

Anataka kupata majibu ya maswali muhimu na zana zake za nguvu za ajabu:
Siku katika maisha yako ikoje? Ni kiasi gani unapata muda wa kufanya kazi kwenda shule, kucheza na kupumzika?
Nguvu za Ajabu-Zana: "siku katika maisha ya ..."






Unapenda nini kuhusu kazi yako, haupendi nini?
Nguvu ya Nguvu-Zana: Ramani ya Mwili



Mtu anapaswa kufanya nini kuboresha maisha yako?
Nguvu ya Nguvu-Zana: Mawa ya Msaada


"Ninatumia taarifa hii kutoa ripoti ya Mkutano wa Dunia juu ya Kazi za Watoto, na nitaipeleka mwenyewe Argentina. Hii inamaanisha kwamba watu wengi watasikia watoto wanaofanya kazi wanasema nini! "Hiyo ni nzuri," nikasema. Kisha akaniuliza kama nilitaka kumsaidia. Alihitaji mtu kuandika kila kitu chini. "Haina shida!, nikasema, na Trixi akatingisha mkia wake. Supermaia akaruka kwa furaha.





Tukiwa na Superautomobile ya Maia, tulikuwa Amerika ya Kusini ndani ya muda mfupi. Huko tulikutana na watoto wanaofanya kazi kutoka nchi saba.

Maria alikuwa mmoja wao. Ana umri wa miaka 13 na anaishi na wazazi wake na ndugu na dada wadogo katika kijiji Peru. Baba yake ni mgonjwa na hawezi kufanya kazi. Kwa sababu hiyo, Maria anahitaji kumsaidia; kabla ya shule, anapaswa kufanya kazi nyumbani, na baada ya shule, anafanya kazi kama mzoa taka. Jumamosi siku nzima! Familia inaweza kununua mchele na maharagwe kwa mshahara wake





— Watoto wengine walitupa sababu nyingine kwa nini wanafanya kazi. Mambo haya yalitajwa pia:


✪ Wazazi / familia wanahitaji msaada ✪ Familia ni maskini, au ina matatizo mengine ✪ Wanataka kuwa na uwezo wa kununua vitu, au kuwa na uhuru zaidi ✪ Wanaweza kulipa ada ya shule ✪ Wanafurahia kufanya kazi ✪ Ni fursa ya kujifunza jambo ✪ Wana hamu ya kuwa na wakati bora baadaye





Watoto katika nchi nane za Asia pia walifurahi kutuambia kuhusu maisha yao ya kazi. Kama Banju kutoka India. Ana umri wa miaka 15 na anaishi na bibi na babu yake. Wazazi wake walihamia mjini kutafuta kazi. Banju husaidia bibi yake asubuhi. Baada ya shule siku za Jumamosi, hufanya kazi katika karakana. Analipwa kidogo sana, lakini anajifunza mengi kuhusu magari. Anafurahia kwa sababu anataka kuwa fundi magari mzuri siku moja, kazi anayoitamani sana kuifanya! Banju anafurahia kupata fedha zake pia. Ili aweze kutumia wakati na marafiki zake.





Watoto wengi hufurahia kazi yao wakati...

☐ watu wanapowatendea kwa fadhili na heshima ☐ watu wanapowasifu kwa kazi zao na kuwaacha wafanye kazi ☐ wanaweza kujivunia kazi zao ☐ wanapata kipato kwa kufanya kazi ☐ huwapa ujuzi na stadi muhimu za maisha ☐ wanaweza kusaidia familia zao na kuwa karibu nao ☐ marafiki na watu wazima wanawasaidia na kuwajali.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mambo ambayo watoto hawapendi kuhusu kazi zao.



Dasha toka Kyrgyzstan hapendi kupuuzwa au kufanyiwa kitu kibaya zaidi. Dasha ana miaka 12 na anaishi na mama yake na kaka yake mjini. Yeye huenda shule asubuhi, na kuuza vitu mitaani mchana. Hukutana na marafiki zake mitaani. Wanafanya kazi pia. Dasha anahitaji fedha kwa ajili ya kununua kalamu, madaftari na vitabu vya shule. Kazi anayofanya inachosha sana; hutembea kwa miguu kila sehemu na mara zote lazima abebe bidhaa zake, lakini Dasha anajivunia. Kwa maana mama yake hana haja ya kutafuta pesa peke yake.

Chochote watoto wanachofanya, popote wanapofanya kazi, hawapendi mambo yafuatayo yanayotokea kazini:

Kusemwa, kupigiwa kelele, kupigwa Majeruhi, ajali Sehemu mbaya ya kufanyia kazi, kazi nzito za kimwili, maamuzi mengi sana ya kufanya, shinikizo kutoka juu, kupumzika kidogo, malipo kidogo Kazi inachosha: jitihada nyingi, malipo kidogo Uchovu Watu hawawapendi Wanafanya kazi peke yake Hakuna wakati wa kusoma




Kenya ilikuwa kituo cha 07 kwenye safari yetu kupitia bara kubwa la Afrika. Tulikutana na watoto wengi sana, lakini kila mmoja wao anaweza kusema kazi ambayo ni sawa kwa mtoto na ambayo sio. Dario (11) anaishi na ndugu zake wawili wakubwa na dada mmoja katika nyumba ndogo kijijini. Kila asubuhi analisha kondoo wa familia. Kisha anaenda shule kwa miguu. Kwa miguu! Lakini si mbali sana. Anajivunia kuwa mwanafunzi. Anapotoka shuleni kuelekea nyumbani hukusanya kuni kwa ajili ya mama yake. Wakati wa mchana anaanza kufanya kazi za shule akiwa nyumbani. Kisha anacheza na marafiki zake hadi muda wa kula chakula cha jioni. "Kazi ni nzuri sana, kwa sababu ni rahisi kufanya. Na nina muda wa kutosha wa kucheza na marafiki zangu ", alituambia.

— Tuliwauliza watoto kuhusu mazingira ya kazi wanazofanya ambayo ni 'Sawa' kwao. Haya ndiyo majibu tuliyopata mara nyingi: —

☑ Rahisi kushughulikia ☑ Salama na salmini ☑ Nyumbani au karibu na nyumbani ☑ Kwa msaada kutoka kwa familia / watu wazima ☑ Haingiliani na mafunzo / kwenda shule ☑ Muda wa kutosha kupumzika na kucheza

Je, ni sawa kwa wavulana na wasichana?




Watoto walikuwa na maoni tofauti! Kuna tofauti ambazo kwa wasichana ni 'SAWA' kama vile kupika, kuosha vyombo, kuchota maji, kutunza ndugu na dada, kutengeneza, kushona na kukata nywele. Wavulana hasa walitaja: kusaidia shambani, kwenye duka au kazi za bustani, kazi nyingine za mikono na ukarabati.





Dario alionekana kufurahia kazi yake. Hata hivyo Farida alituambia hadithi tofauti. Familia yake ilikimbilia Jordan kutoka kwenye vita huko Syria. Wazazi wake wanapata shida kupata kazi. Wakimbizi hawaruhusiwi kufanya kazi. Hata hivyo, watoto wakimbizi wanapewa kazi, ingawa ni marufuku. Kwa kuwa ni nafuu kuwalipa kuliko wafanyakazi watu wazima na wanaweza kukimbia mara moja wakati wa ukaguzi. Farida ana miaka 15 na binti mkubwa. Kwa hiyo husaidia familia yake. "Ninafanya kazi siku sita kwa wiki kwenye shamba na kuchuma nyanya. Mara nyingi nacho yangu huuma kwa sababu ya dawa za kuua wadudu. Na jua huchoma ngozi yangu, "Farida anasema. Ana huzuni sana kwa sababu hawezi kwenda shule hapa, na hana muda wa kucheza na marafiki zake.





— Tuliwauliza watoto kuhusu hali za — kazi ambazo si 'SAWA' kwao. Majibu ya kawaida yalikuwa:

- Si salama, au kuna hatari ya kupata ajali au kujeruhiwa
- Bado ni wadogo au dhaifu sana, na kazi ni ngumu sana
- Ni marufuku
- Ni hatari sana kwao
- Inaingiliana na masomo yao
- Malipo ya chini, hakuna malipo yoyote, au saa nyingi za kazi
- Dini au utamaduni wao hauruhusu



Tulizitembelea nchi 36 na tulikutana na watoto 1822. Wote hufanya kazi kwa njia nyingi tofauti. Kwa wengi wao, hii ni jambo jema. Wanathaminiwa, wanajifunza kitu katika kazi na wanaweza kujivunia kile wanachofanya. Kwa wengine wengi, hata hivyo, changamoto ni nyingi kuliko mema. Kuna sababu za kazi kuwa nzuri au mbaya.

Kuna mambo ya ulinzi! Mtoto...

wanaweza kwenda shuleni kwa ukawaida

•

ni mwanachama wa muungano wa watoto

•

anaruhusiwa kushiriki katika maamuzi kuhusu kazi zao

•

lazima afanye kazi nyepesi tu

•

anaonyeshwa upendo

•

matunzo na msaada

•

ana wazazi wenye kazi nyumbani kwao

•

Kuishi kwenye nchi inayochangia elimu na kujenga miundombinu mingine muhimu na wezeshi

Na sababu za hatari! Mtoto...

anapaswa kufanya kazi ngumu au hatari

•

analazimishwa kufanya kazi

•

inabidi afanye kazi usiku

•

anafanya kazi mitaani

•

hawakai na wazazi wao

•

analazimika kufanya kazi kwa saa nyingi

•

anaishi katika nchi hatari

•

ilibidi familia yake ikimbie



Mei 10

Mpendwa shajara, Nimerudi baada ya safari ya nzuri sana katika nchi nyingi (kwa wakati barabara wa siku ya kuza-liwa kwa Mama)! Nilikutana na kufahaamiana na watoto wa kipekee. Walituonyesha kazi na maisha yao na watoto wanaofanya mambo nazuri ajabu. Salamu ya maua na walitupa 'Maua ya Msaada' ujumbe wake ni kwa watu wote duniani ambao wanaweza kusaidia watoto wanaofanya kazi ili kuboresha maisha yao.





Njia nyingi za kutatua matatizo hayo

Ni muhimu kujifunza kutoka kwa watoto na familia wapi na jinsi wanavyoishi, na kwa nini watoto wanafanya kazi. Kisha tunaweza kuelewa kwamba wana maisha tofauti sana. Kwa hiyo, ufumbuzi wa aina nyingi unahitajika. Suluhisho sahihi kwa kila mtoto.

Kupambana na umaskini

Serikali zinapaswa kufanya mengi zaidi kwa familia. Wanapaswa kupambana na umasikini, kutengeneza ajira na kuwasaidia wazazi ikiwa ni wagonjwa au hawawezi kupata kazi yoyote. Kisha watoto hawatahitaji kufanya kazi chini ya hali ya hatari, na wanaweza kwenda shule na kucheza wanapopata nafasi.

Kuimarisha haki za watoto

Watoto wana haki ya kutoa maoni yao, kujulishwa, kushiriki, na kukusanyika. Kila mtu anapaswa kuelewa hilo. Hasa wale ambao wana uhuru wa kusema katika ulimwengu wa watoto: familia, shule, kazini, katika jamii na siasa. Kila mtu anapaswa kusikiliza maoni ya watoto na kuyachukulia kwa uzito.

Fanya iwezekane kupata elimu

Watoto wana haki ya kupata elimu. Watoto wote! Watoto wanaoishi miji, vijijini, watoto wa wakimbizi, na hata wale wanaoishi mbali. Kila mtoto anaweza kwenda shule nzuri - bila kulipa! Vijana wanapaswa kuwa na uwezo wa kujaribu kazi nzuri na kujifunza ustadi.

acha unyonyaji!

Watoto wanapaswa kulindwa kutokana na kazi hatari na zenye madhara. Kwa kazi ambayo wanapaswa kufanya dhidi ya mapendezi yao, na kazi yenye mshahara mdogoau kazi zilizokatazwa. Ni lazima kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

Linda watoto dhidi ya jeuri

Watoto wanapaswa kulindwa dhidi ya kutendewa kijeuri. Iwe ni katika familia, shuleni, kazi au popote pale. Mifumo ya ulinzi wa watoto lazima iundwe na kufadhiliwa ili kusaidia hili.



Wewe ni nani? Je, wewe hufanya kazi pia? Tuambie kuhusu wewe!

Jina langu:

Umri wangu:

Kazi yangu:


Siku yangu:

Familia yangu:

Rafiki zangu:

Ndoto zangu:


Andika ujumbe wako kwa kila ntu ambaye anaweza kufanya kazi na maisha yako kuwa bora katika Maua ya Msaada.






Trixi ana ujumbe kwa Paul pia:
Hebu tucheze mchezo wa 'kutupa fimbo' na kisha ukune mgongo wangu, sawa?

Maelezo



Maelezo



Shukrani za pekee ziende kwa watoto na vijana 1822 walioshiriki waliotoa maoni yao na sisi na kuwezesha utafiti huu. Shukrani zaidi ziende kwa wanachama wote wa kamati za ushauri wa watoto waliotuunga mkono kama washauri, wachambuzi na watetezi.



Imprint

Mchapishaji
Kindernothilfe, Ujerumani
Terre des Hommes International Federation

Kubuni & Dhana
mañana kreativbüro, Düsseldorf
www.maniana-design.de
Sara-Lena Göbel & Daniel Bolay

Michoro
George Popov, Düsseldorf

Msimulizi
Christian Matzerath, Düsseldorf
akisaidiana na Anne Jacob, Kindernothilfe

Imefadhiliwa kwa ushirikiano kati ya

Federal Ministry
for Economic Cooperation
and Development

Kijitabu hiki kinachofaa watoto ni sehemu ya machapisho ya kampeni ya kimataifa na mradi wa utafiti wa "Ni Wakati wa Kuongea! - Maoni ya Watoto juu ya Kazi ya Watoto" na inategemea ripoti rasmi ya utafiti kuhusu mazungumzo yaliyofanywa na watoto na vijana wanaofanya kazi katika nchi 36.

Maelezo zaidi juu ya mradi na ripoti ya utafiti:
www.time-to-talk.info



kinder not hilfe

Terre des Hommes
International Federation